

SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



EU UNIVERSE
AWARENESS

Nyota Zilizostaafu na Kinyago!



Mara nyingi watu wakistaafu huchukucha fani mpya ili kufidia mda wao, kama vile kuchora au kuvua samaki. Wanaastronomia katika siku za karibuni wameziona nyota mbili zilizostaafu (ziitwazo mbilikimo weupe), katika kiini cha nebula ya kupendeza iliyochukua sura ya kinyago! Maada za rangi nyekundu zinachochirizika kutoka katika kila kona ya nebula hii zimejikunja katika mfumo wa S baina ya nyota hizi mbili za zamani.

Nyota kama Jua ikiishiwa nishati, inaanza kubomoka ndani kwa ndani. Maada zilizopo katika kiini chake huishia kugandamizwa katika tone dogo lenye uzito mkubwa. Tone hili dogo huitwa mbilikimo mweupe. Nyota hiyo pia hypoteza gamba lake la nje la gesi na kuele angani. Gesi ambazo hutengeneza planetari nebula – ambayo ni mawingu ya kupendeza yanayozunguka mbilikimo mweupe, kama yalivyoonyeshwa katika picha.

Sio jambo lililozoleka kwa wanaastronomia kuziona nyota mbilikimo nyeupe zikiwa zinazungukana katika mfumo unoaitwa mfumo pacha na wanaastronomia. Pia ni aghalabu sana kwa nyota hizi kuwa karibu karibu sanal Wanaastronomia wanatarajia nyota za mbilikimo weupe kuchukua miongo kadhaa ili kukamilisha mzunguko mmoja kuzungukana, lakini kwa hizi mbili huchukuwa muda wa kama siku moja hivi!

Kadri nyota hizi zinavyozidi kuzungukana, huathiri utupwaji wa maada kutoka katika kiini chake, na kuzisababisha kujipinda katika upo la kuvutia la S.Wanaastronomia wametumia miaka mingi wakistaajabu ni kwa jinsi gani michirizi hii ya kupendeza inavyotengenezwa na sasa wameweza kujual

COOL FACT

Kipande cha mbilikimo mweupe change ukubwa na dunge la sukari kinaweza kuwa na uzito sawa na kiboko!



More information about EU-UNAWE Space Scoop: www.eu-unawe.org/kids/